

IGUNGA YA MAENDELEO



Igunga yaubeba mkoa kwa ubora wa Miradi.



Ndg Shaka Hamdu Shaka, amesema kuwa tangu alipoingia Igunga ameona namna miradi ilivyosimamiwa kwa kiwango cha juu sana. Amewataka viongozi wengine wafike igunga kwa ajili ya kujifunza. Shaka alipongeza viongozi wa

chama na serikali kwa kusimamia fedha za maendeleo zinazoletwa na mama yetu mpendwa Mhe:Samia Suluhu Hassani Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Akiwa Kata ya Nanga 20/8/2022,Shaka akaongeza kusema kuwa

Igunga itumike kama SHAMBA DARASA, kwa viongozi wengine kuja kuifunza Thamani ya fedha na miradi yenyewe muonekano wake inavyopendeza.

IGUNGA YA MAENDELEO



uk 2

Karibu tena Igunga ndg Shaka H. Shaka Katibu Halmashauri Kuu ya CCM Itikadi na Uenezi



WAKUFUNZI WA MAENDELEO (SHAMBA DARASA) IGUNGA.
Kushoto Mhe:Sauda Mtondoo
Mkuu wa Wilaya ya Igunga. Kulia Bi:Fatuma O. Latu Mkurugenzi
Mtendaji wilaya ya Igunga. Karibuni viongozi kujifunza Nidhamu
ya Fedha za maendeleo ya wana-nchi(Shaka H. Shaka Katibu itikadi
na Uenezi Taifa CCM).



Mbunge wa Igunga kujenga ofisi za CCM kila Kata.



Mhe: Nicholaus Ngasa amemwambia Katibu wa Itikadi na uenezi Taifa, kuwa anampango wa kujenga ofisi za chama kila kata. Ngasa amesema ofisi hizo zitajitosheleza kimi-

undombinu, ikiwa ni pamoja na Ukumbi wa mikutano na Mageti mawili ya biashara, ili kuongeza vitegauchumi vya chama cha mapinduzi (CCM). Kitabu chenye picha za mu-

onekano wa majengo hayo yatakayojengwa amemkabidhi Nd-g;Shaka H. Shaka.





Rais Samia aupiga mwingi kila sekta jimbo la Manonga na jimbo la Igunga.



Mhe:Seif Gulamali Mbunge wa jimbo la Manonga, ametoa shukrani za dhati kwa niaba ya wananchi kwa Mhe:Samia Suluhu Hassani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,k-

wa Kuwapatia Fedha nyingi za maendeleo katika miradi ya Elimu, Afya, Maji na Barabara, Shukrani hizo amezitoa mbele ya katibu wa Itikadi na uenezi Ndg: Shaka H. Shaka. Pia Gulamali

ameiyomba serikali itengeneze barabara ya kutoka Ndala, Simbo, Nkinga, Ziba hadi Choma kwa kiwango cha Lami yenye urefu wa kilomita 83.





Shaka: nitakuwa mpambe wenu kuwapigia debe mpare fedha za maendeleo.



Hayo ameyasema Ndg: Shaka H. Shaka baada ya kufurahishwa na hali ya maendeleo alioyaona kwenye majimbo

mawili ya Igunga na Manonga, Kiongozi huyo amewaaahidi viongozi wa chama na serikali kuwa atarudi tena kuzunguka

kila kata kuimalisha chama cha Mapinduzi(CCM).

